Femina HIP

# Si Mchezo!

Mei - Juni 2013 Toleo Na. 66

Haliuzwi


## KATUNI




# Dawa ya deni Kulipa

ISSN: 0856-8995




Si Mchezo! Huzalishwa na kusambazwa.

Si Mchezo! husambazwa.

Lilikozalishwa toleo hili.

Femina HIP
Jarida la Si Mchezo!

**Mkurugenzi Mtendaji**
Dr. Minou Fuglesang

**Mkurugenzi wa Habari**
Amabilis Batamula

**Meneja Machapisho**
Jiang Alipo

**Mhariri Mkuu**
Majuka Ololkeri

**Waandishi**
Raphael Nyoni
Rebeca Gyumi
Betty Liduke

**Washauri**
Timu ya Femina HIP

**Meneja Uhusiano**
Lilian Nsemwa

**Katuni na Usanifu**
BabaTau, Inc.

**Mpiga Chapa**
Jamana Printers Ltd

**Usambazaji**
EAM Logistic Ltd
Femina HIP na Washirika

Si Mchezo! limefanyika kwa hisani kubwa ya Serikali za Sweden (Sida), Denmark (DANIDA), HIVOS, RFSU, TWAWEZA na JHU-CCP/TCCP

Yaliyomo humu ndani ni jukumu la Femina HIP na hayawakilishi maoni au mitazamo ya wafadhili.

**Wasiliana nasi kwa:**
S.L.P. 2065, Dar es Salaam
Simu: (22) 212 8265, 2126851/2
Fax: (22) 2110842
email: simchezo@feminahip.or.tz
Si Mchezo! huchapishwa na Femina HIP.
**Sms: Andika SM acha nafasi andika maoni yako kisha tuma kwenda 15665**

# YALIYOMO




4 **Stori Yangu:** Dawa ya deni kulipa
6 **Mambo Mapya**
8 **Hadithi ya Picha:** Nani ajuae?
12 **Je, Wajua:** Mabadiliko yanaanza na wewe
14 **Sauti yangu**
16 **Burudani:** Kubum kubam!
18 **Ruka Juu:** Umoja ni nguvu itumieni
20 **Nguvu za mwanamume:** Baba kijacho linda chako
21 **Nguvu za mwanamke:** Kweli inawezekana
22 **Chezasalama:** Mwili wako maamuzi yako
24 **Katuni**
27 **Ukweli wa mambo:** Mambo haya si mambo
28 **Sema Tenda:** Fungu hili limekaaje mazee?
31 **Ushauri**

# TAHARIRI

Mzigo mpya ndio huu umetinga kitaa. Tulitembelea Jiji ambalo madini, utalii na rasilimali za ukweli Tanzania ndipo zilipo. Mambo yaliyopo ndani ni elimu tosha kukuelimisha juu ya miradi ya maendeleo ya vijana katika Halmashauri zetu. Tulipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa vijana wa Sokoni II Art Group. Pamoja sana watu wangu. Peruzi upate uhondo

***Majuka***



# Dawa ya deni kulipa

Katika mambo ambayo siku zote huwa nayaheshimu ni makubaliano niliyowekeana na mtu. Hii imenifanya kuwa mfano mzuri kwa vijana wenzangu hapa Sekei. Nawapa elimu kwenye kikundi ili tuwe makini katika kujipanga kimaisha. Kuishi kwa malengo kumenisaidia kufika hapa nilipo nikiwa na matumaini makubwa ya kupiga hatua zaidi.

Ukifika mitaa ya Sekei, Arusha ukaulizia Joseph William, usishangae ukanipata kwa urahisi tu, napenda kujichanganya. Hapo ndipo nyumbani, ndipo nilipozaliwa miaka 29 iliyopita.

Moja ya mambo ambayo nimewashirikisha vijana wenzangu siku za karibuni ni ufuatiliaji wa mfuko wa maendeleo ya vijana katika Wilaya yetu. Kikundi chetu cha sanaa, Sokoni II, kimepiga hatua na sasa tuko mbioni kupata mkopo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha baada ya kutimiza vigezo vinavyotakiwa. Tunafukuzia.

Nakumbuka pia baada ya kumaliza darasa la saba, tuliungana vijana watano tukaomba mkopo wa biashara, tukapata. Kila mmoja alitakiwa kufanya shughuli itakayomuwezesha kurejesha mkopo huo kwa muda tuliokubaliana kimkataba. Nilianza biashara ya kuuza nguo za mtumba, kwa makini na uaminifu. Nilijua nikikosea taratibu za mkopo naweza nikakosa fursa zaidi ikiwamo kupewa mwingine. Nilikuwa nimeshaona watu wengine wakinyimwa mkopo zaidi au hata kufilisiwa.

Nilipambana na biashara huku nikirudisha



*Joseph William akiwa nyumbani kwake huko Sekei, Arusha.*


mkopo huo. Biashara iliyumba kwa uchache wa wateja. Nilituliza akili na kutafakari la kufanya ili nipate faida zaidi. Tulifanikiwa kurudisha mkopo ule wote. Niliomba mkopo mwingine nikaiboresha biashara yangu. Nilikuwa nikipata pesa, naigawa; kiasi naweka na kiasi natumia. Nilijinyima na kuwa mwangalifu katika matumizi. Nikafanikiwa kurudisha mkopo wote na kumudu kufanya biashara bila deni. Baadaye nilibadilisha



biashara na kununua bodaboda ambayo naikodisha huku nikijishughulisha na biashara ya kuuza bidhaa za urembo. Pesa za kukodi pikipiki naziweka benki na najitahidi nisiziguse hadi ziweze kununua nyingine.

Nimejenga nyumba na nina mke na mtoto mmoja, tunategemea biashara hii hii. Kwa kuwa nimepitia changamoto katika kuhakikisha narudisha mikopo yote niliyokopa kwa wakati, niliamua kutoa elimu kwa vijana wenzangu hapa Sekei. Baadhi yao walinisikiliza, na wamepiga hatua kwenye maisha yao. Kikubwa ni kuheshimu makubaliano na kusimamia uamuzi uliyojiwekea bila kubadilishwa na vishawishi vibaya kama ulevi.

Ushauri wangu kwa vijana ambao wanahitaji mikopo, wabuni shughuli ya kufanyia mkopo huo ambayo itawawezesha kulipa.







*JCB akichana mistari huko Arusha.*

## Wasanii R-Chuga moto

Ilikuwa ni vuta n' kuvute siku ya uzinduzi wa Jiji la Arusha pale waandaaji wake walipoalika msanii kutoka Dar kwenda kutumbuiza na kuwaacha wasanii wa jiji hilo maarufu kama R- chuga wabaki katika viti vya mashabiki.

Baadhi ya wasanii kutoka jiji hilo jipya hawakuelewa somo, na wakataka waeleweshwe kwa nini hawakualikwa, wakati Arusha ni kwao na shughuli inawahusu?

Mwisho wa siku kikaeleweka kwa wasanii wa Arusha kupanda stejini na kuzindua jiji lao kwa shangwe.

Ndivyo inavyotakiwa, ukiona haki yako inaporwa unakwenda kwa wahusika kuhoji inakuwaje, kama walivyofanya wasanii hawa wa Arusha. Kama kuna tatizo linarekebishwa na haki inatendeka. Sema, Tenda!

## Wanawake changamkeni

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu akihutubia wananchi wa Jiji la Arusha katika Siku ya Wanawake Duniani ambayo inaadhimishwa kila mwaka. Waziri Ummy aliwataka wanawake kujiamini katika utendaji wao na kuchangamkia fursa mbalimbali ili kuikwamua jamii.

Kilele hicho kilifana sana kwani kinamama walionyesha ustadi wao kutengeneza bidhaa mbalimbali na kuandaa vyakula vya asili kama vile ngararumu, Pamoja na kuuza bidhaa hizo kwa watu waliohudhuria.





## DSW watoa elimu ya ujasiriamali Arusha

Mhariri wa Jarida la Si Mchezo!, Majuka Ololkeri akitoa maelezo kwa wanawake wajasiriamali juu ya ujio wa timu ya Si Mchezo kwenda kuzalisha jarida la Si Mchezo katika halmashauri ya wilaya ya Arusha mwezi March mwaka huu.Wananwake hao walikuwa kwenye mafunzo ya yjasiriamali yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la DSW wakishirikia na halmashauri ya wilaya ya Arusha.





## Somo la ujinsia

Theresia Eliasi, mwalimu wa Chuo Cha Maendeleo ya jamii jijini Arusha ,akitoa somo la ujinsia kwa wawakilishi wa kina baba na kina mama kutoka maeneo mbali mbali ya jiji la Arusha ili kuleta mabadiliko toka ngazi ya familia hadi taifa.


Changamoto ilitolewa kwa kina baba kukubali kushirikiana na kina mama bega kwa bega katika kuleta mabadiliko, badala ya kuziacha sera hizo mara tu wanapotoka katika milango ya kumbi za semina.



## Sekei ni noma!

Baada ya kuona adha ya maji iliyowakumba kwa muda mrefu, wananchi wa Sekei wakaona 'isiwe tabu; "kwani tukiunganisha nguvu na umoja hatuwezi kumaliza hili tatizo?" kwa pamoja wakachimba kisima.

Kisima hiki kinasambaza maji kwa wanajamii kwa ratiba maalumu ambayo wamejipangia  ili kutoa nafasi kwa kila mmoja kupata huduma hiyo muhimu katika maisha ya mwanadamu.
Mtu akizingua kuhusu utaratibu, kijiji kinamchukulia hatua. Hakuna 'overtake hapo' .
Unajua nini? Haya ndiyo mambo yanayotakiwa, siyo kila kitu unalalamika kwa serikali, hata yale unayoweza kurekebisha mwenyewe. Ukiona mambo si mambo katika eneo lako, kama vipi unakusanya nguvu na kurekebisha kama hawa wenzetu wa Sekei. Eeeh unadhani wangesubiri maji yangekuja lini? 'Change' ni mimi.



*Mhariri wa Jarida la Si Mchezo, Majuka Ololkeri (kulia)akiwa na baadhi ya wanakijiji wa Sekei karibu na tanki lao la maji*

# pata potea


wilayani zimetengwa pesa kwa ajili ya kusaidia vikundi vya maendeleo ya vijana. Tangazola kutoka kwa pesa hizo limeandikwa. Mchuano mkali ni kati ya kikundi cha Kazamoyo na Mteremko. Je vigezo na masharti vitazingatiwa au vitakiukwa? Fuatilia







MTEREMKO WANATAARIFIWA NA AFISA
VICENT HIVI KILE KIKUNDI CHENU BADO KIPO?
BADO KIPO MKUU!
NAHITAJI TUONANE HARAKA
KAZAMOYO WAKIPANGA MKAKATI
---HII NI FURSA YETU KWANI HAKUNA KIKUNDI KIZURI ZAIDI YETU
MMH! NNA WASIWASI NA URAFIKI YULE AFISA NA VICENT
MTEREMKO
MAOMBI YAKO HAYAJAKAMILIKA. MBONA HAMNA NAMBA YA USAJILI WA KIKUNDI NA SAHIHI ZA WANACHAMA?
MBONA MKUU HAKUNIAMBIA HIVYO? NGOJA NIMPIGIE
NIMELETA YALE MAOMBI LAKINI NAAMBIWA SIJUI KUNA VITU NATAKIWA KUVILETA
NIPE NIONGEE NA HUYO MSICHANA
VICENT AKISAIDIWA NA AFISA
KAZA BUTI NITAKUSAIDIA
BAADA YA MIEZI KADHAA
KIKUNDI CHENU HAKIJAFANIKIWA KUCHAGULIWA, LAKINI MSIKATE TAMAA
TUMEKOSEA WAPI KWANI?
MMH! HAWAJACHAKACHUA KWELI?


BAADA YA KUSAIDIWA NA AFISA WILAYANI KIKUNDI CHA MTEREMKO WAMEPATA MKOPO NA KILE CHA KAZAMOYO WAMEPIGWA CHINI. IKAZI KWAO MTEREMKOP KUTEKELEZA MRADI TUENDELEE NA STORI HUENDA TUKAJUA MBELENI.
KAZI KWENU SASA KUWEZA KUREJESHA MKOPO HUU KILA MWEZI NA KWA WAKATI
MTEREMKO WAKIJAZIA FOMU BAA
TUJAZE HIZI FOMU ZA MKOPO KUWA TUMETUMIA PESA
JE,WAKIJA KUANGALIA MRADI TULIOSEMA TUNAFANYA?
HIYO NI HABARI NYINGINE...
MKUU UMECHELEWESHA KULIPA DENI LAKO, TAFADHALI WAKILISHA HARAKA
HAINA TATIZO MKUBWA
SAMAHANI KWA KUCHELEWESHA MALIPO, LAKINI MAMBO YAMEBANA
KWA VILE NI WEW TU, LAKINI HII PESA NI NDOGO
AKIELEKEA ZANZIBAR
MPAKA MKWANJA UNAISHA SIJAPANDA NDEGE? HAIWEZEKANI!


YAANI MKUU HILO SIO TATIZO
KWA MIKAKATI NILIIYOJIWEKEA, SITAKUANGUSHA MKUBWA
LEO TUKUTANE PALE BIG G PUB TUJIPONGEZE
HAHAHAH HAPO MALAIKA HAZINGUI TENA
MBINU ZAKO ZA HATARII!
WASWAHILI WANASEMA KUKOPA HARUSI KULIPA MATANGA. SASA INABIDI WANAKIKUNDI WA MTEREMKO KUONYESHA MRADI 'FEKI'
HIVI SIKU AKIGUNDUA KUWA SI LA KWETU ITAKUWAJE?
HUU NDIO MRADI WETU
MKIJITAHIDI ITAWALIPA
WEWE NDIYE ULIYEWADHAMINI HAWA VIJANA, SASA NATAKA WAMALIZE DENI WIKI HII, LA SIVYO ITAKULA KWAKO
BOSI TAFADHALI, NIPE MUDA WA KUWAFUATILIA HUKO OFISI YA WILAYA
MMH! JAMAA NDO AMETOWEKA NA BOSI ANANIVUTA SHATI HIZI PESA SIJUI ITAKUWAJE

# Mabadiliko yanaanza na wewe

Kilichotokea kwenye mchezo huu ni moja ya vituko vinavyotendeka katika sehemu nyingi ambazo zabuni hutangazwa lakini mchakato wa kumpata mshindi unakuwa mchezo wa kuigiza. Tumaini la kikundi cha Kazamoyo ilitoweka baada ya kuambiwa kuwa hawakufanikiwa kupata mkopo kutoka kwenye mfuko wa maendeleo ya vijana wilayani kwao. Walikuwa na uhakika wa kupata kwani wanajua hawana mpinzani katika eneo lao.

## Siri iko hivi

Tulipotembelea wilaya mbalimbali, vijana wameonekana kukerwa na baadhi ya 'wakubwa' wanaowatumia vibaya vyeo vyao na kuwanufaisha wachache kitu ambacho inawanyima fursa za kujifunza na kujiendeleza. Mizizi ya rushwa iliyoota katika jamii sasa inashamiri kwa mbinu za kila aina. Vijana wanajitahidi kuwa karibu na viongozi lakini kama walivyosema 'usipokunjua' mkono kikundi chako kitaishia kwenye maonyesho ya kwenye ratiba.




## Chukua hatua

Kama vijana wetu hawatakuwa na imani kwa viongozi wao ni hatari kwani itadidimiza vipaji vya vijana na kuwakatisha tamaa wengine wanaotaka kujiunga na vikundi vya maendeleo. Tujenge urafiki na vijana katika wilaya zetu ili wajue vipaji vyao na kupata ushauri pia. Tunapowanyima fursa vijana waliojitahidi kukikuza kikundi chao, tunapoteza kundi muhimu katika jamii

## ☺ Kumbuka

*Vijana ni haki yenu kufuatilia bajeti ya maendeleo ya vijana katika wilaya zenu na kujua matumizi yake. Kwa kufanya hivyo mtaidhibiti mianya ya rushwa.*










fema RADIO

# RUKA jUU

## Young Farmers in Business

Femina HIP

RUKA JUU! fema


Kuanzia Machi 2013,
Femina itakuletea Ruka Juu TV show
Usicheze mbali na luninga yako

**ITV kila Jumamosi saa 1 usiku**

**TBC1 Kila Jumapili saa 4 usiku**

Funguka shambani peta maishani na Fema Radio.
**RFA kila Jumatatu saa 2.45 usiku**
**TBC FM kila Jumanne saa 4 usiku**

# SAUTI YANGU





**Kama una chochote unachotaka kusema tuandikie ili upate fursa ya kuwaelimisha wengine**

Maoni yaliyotolewa katika ukurasa huu ni ya wasomaji, si lazima yalingane na msimamo wa Femina.

## Watoto waishio mitaani kunani?

Katika maisha ya sasa kila kitu kimekuwa juu. Hali hiyo inafanya maisha ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu kuwa na wakati mguu zaidi. Nikiwa kijana naomba serikali itafute mbinu ya kupunguza watoto hawa mitaani. Wasaidiwe katika suala la elimu na malazi pamoja na kutoa elimu kwa wazazi na walezi wanaowalea. Tujitahidi watoto hawa wapate elimu ili baadaye waweze kuishi katika mazingira mazuri.


*Evershine George*
*Arusha*




## Mfano gani huu?

Inakera sana tabia ya baadhi ya vijana ambao wamezoea kunywa pombe halafu kutukana mitaani, kiasi cha mtoto wa darasa la kwanza anakariri na kuyajua matusi yote, kisha kuyarudia na jamii kulalamika kuwa watoto wa siku hizi hawana maadili mema. Sisi vijana ndiyo chachu ya mabadiliko, inabidi tubadili hizi tabia ili kufanikisha mabadiliko hayo na kutengeneza jamii yenye maadili. Kwani jamii njema inaanza na watoto wema.

*Ignasi Roberty*
*Arusha – Sekei.*





## Matumizi mabaya ya 'facebook'

Napenda kuliongelea hili hususani kwa vijana wa shule. Wengi wa wanafunzi wa 'kidigitali'wanatumia muda wao mwingi kuingia kwenye facebook na mitandao mingine ya kijamii kwa muda mrefu badala ya kutumia muda huo kwa kujisomea. Hii inawasababishia kushindwa kusoma kwa bidii na kufanya vibaya wanapopewa majaribio na mitihani katika masomo yao. Nawashauri wanafunzi wasome kwani elimu haina mwisho. Kufeli shule siyo kufeli maisha, lakini kaeni mkijua huku mtaani moto unawaka.

*Magreth Anaely*
*Arusha*

## Tumeshajifunza jamani

Tunadharaulika sana sisi wasichana tuliopata mimba katika umri mdogo. Tunaonekana kama vile sisi ndiyo wakosaji pekee, kumbe tulikuwa hatujapatiwa elimu ya kutosha kuhusiana na masuala ya ujinsia, mahusiano na afya ya uzazi, lakini sasa tumeshaipata. Kutenda kosa si kosa ila kurudia, tunajikung'uta vumbi na kusonga mbele. Kwa sasa tunajitahidi kwenda kutoa elimu kwa wenzetu ili wasirudie makosa tuliyotenda dada zao. Yangu ni hayo tu!

*Judith Akyoo,*
*Arusha*






Wewe pia unaweza kulonga na vijana wenzako. Tuandike maoni, ushauri, vichekesho,maswali nk, weka anuani yako na tuma ukiambatanisha na picha yako kwa **Mhariri, Jarida la Si Mchezo!, S.L.P ٢٠١٥ Dar es Salaam. simchezo@feminahip.or.tz** Au tumbukiza katika boksi la Si Mchezo! kama lipo katika eneo unaloishi.

# Wazazi nipendeni yazungumza na Tina Pius

## kuhusu Kupata mtoto bila Maambukizi



"Watu wengi hudhani kuwa kupata maambukizi ya VVU ni mwisho wa maisha. Mtazamo wangu ni kinyume na fikra hizi potofu kwa kuwa mimi ninaishi maisha bora na yenye furaha tele."

Nina umri wa miaka 32 na ninaishi katika wilaya ya Karatu iliyopo mkoani Arusha

Nilifunga ndoa mwaka 2000 na kufanikiwa kupata mtoto wangu wa kwanza mwaka uliofuata. Alikuwa ni mtoto wa kiume na tulimpa jina la Arnold. Kwa wakati huo mimi na mume wangu tuliishi katika maisha yenye furaha na upendo.

Mnamo mwaka 2008, niligundua kuwa mume wangu ana mahusiano na mwanamke mwingine tofauti na mimi. Bila hata kuwa na aibu, yule mwanamke alianza kutangaza kwa jamii inayotuzunguka kuwa ametuambukiza mimi na mume wangu VVU. Niliposikia uvumi huo nilimuuliza mume wangu kama ni ukweli. Cha kustaajabu, siku chache baadaye mume wangu alitutelekeza mimi na mtoto.

Muda mfupi baada ya kutengana na mume wangu niligundua kuwa nina ujauzito na nilienda moja kwa moja katika kliniki ya afya ya uzazi na mtoto. Nilipofika kliniki kwa mara ya kwanza muuguzi alinishauri nifanye kipimo cha VVU na nilipofikia miezi mitano ya ujauzito wangu nilifanya kipimo hicho na niligundulika kuwa na maambukizi ya VVU. Niliingiwa na hofu kubwa ya kupata mtoto aliye na maambukizi ya VVU na nililia kwa uchungu mkubwa.

Nashukuru sana kwa ushauri nasaha nilioupata kutoka kwa muuguzi aliyenihudumia kwani ulinipa tumaini kubwa la kuendelea na maisha kama kawaida. Kwa ushauri huo niliweza kuikubali hali yangu na wauguzi walinihakikishia kuwa naweza kujifungua mtoto asiye na maambukizi ya VVU kwa kupitia ufuatiliaji mzuri wa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto zitolewazo bila malipo yoyote katika vituo vya afya.

Moja kwa moja nilianzishiwa dawa za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Nilifuatilia vizuri ushauri niliopewa na matabibu na waaguzi walionihudumia. Hii ilinifanikisha kupata mtoto asiye na maambukizi ya VVU mnamo mwaka 2009. Nilimwita mtoto huyo Joshua.

Baada ya kujifungua Joshua alipatiwa dawa ya dozi ya mara moja ya "Niverapine" ya kuzuia maambukizi ya VVU kwa watoto. Kupitia ushauri wa wauguzi niliamua kuchagua njia ya kumnyonyesha mtoto maziwa yangu bila kumchanganyia chakula kingine chochote. Joshua alinyonya maziwa yangu kwa miezi minne tu na nilimwachisha na kumuanzishia maziwa ya ng'ombe.

Joshua alipotimiza umri wa miezi miwili, nilimpeleka tena kituo cha matibabu na huduma (CTC) ili afanyiwe uchunguzi wa maambukizi ya VVU nashukuru hakukutwa na maambukizi ya VVU. Nilirudia kipimo hicho akiwa na umri wa miezi sita, pia hakukutwa na maambukizi.

Ninafuraha sana kumuona mwanangu Joshua ana miaka minne (4) akiwa na afya njema. Kupitia shirika la EGPAF, naishukuru serikali yetu kwa kuwezesha huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto pamoja na huduma za matibabu kwa jumla katika Kituo cha Afya cha Karatu. Ninaamini kuwa mimi na Joshua tutaishi maisha marefu na kutimiza malengo yetu.

Kupata mtoto bila maambukizi inawezekana!!

***Tuma SMS neno "mtoto" BURE kwenda* 15001 *kwa taarifa zaidi***

USAID Kutoka kwa watu wa Marekani · Center for Communication Programs · maisha · Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii · mHealth Tanzania Public Private Partnership · USAID CDC President's Malaria Initiative · Tanzanians and Americans in Partnership to Fight HIV/AIDS



**Wimbo:** Kubum kubam
**Wasanii:** Niki wa pili





***Utangulizi***

*Yeah, it's river baby, Nako to Nako baby,*
*Daz Knowledge (Daz knowledge) the Aaa city dream*
*Let's go*

***Ubeti 1***
*Hii michano sio muchano kina rabadaba*
*Punchline kama vyumba kwenye maktaba,*
*Na break kama news get ready kwenye TV,*
*Na break ma injury bila news wala GV,*
*nipo na Daz Knowledge*
*Pen and paper it's time to get college,*
*Sinukii pafyumu wala sinuki jasho,*
*Nani anafyum uswazi hakuna mipasho*
*Kuna mererani, ngome jela na uraiani,*
*pembe tatu za maisha*
*R back Tangara be KRS one and siwezi be careless one,*
*Kama kufanya sifanyi matusi, kama kuchana nachana sichani ku diss*
*Watumishi watakatifu wanawatumishi ma bodyguard,*
*na vibaka wanalindwa na hirizi za jadi,*
*unapanda mbegu juu ya mbegu eti kisa nyapara?*

***Kiitikio x 2***
*Nani anafyum uswazi hakuna mipasho,*
*Hizi ni ngumu kwenye booth sokoni commercial*
*Hizi ni bum kubam, bu bu kubam*
*kubum kubam, bubu kubam*

***Ubeti 2***
*Hapa nipo natoa maji kwenye kiu,*
*sex figure Fatuma ndio chenyewe kiu*
*kiungwana mangaribi sara rescue, kata karateka Encarta is you,*
*nyie balloon kwenye parachute, wote ni puto nyie katuni kama penseli,*
*kichwa ufuto, platoon zinakuua kwenye booth now,*
*ukweli unakita kwenye chup waaaoh!*
*Siwezi kiss kwenye mbingu naikiss ardhi, ntashuka kwenye ardhi kuelekea mbingu, kifo cha mwenye haki honeymoon*
*bila kanisa kuna misa kwenye hali duni,*
*Naibuni rap, naitune swagga, mpo flat nyie si kama flat za maghorofani,*
*Mpo fat nyie si mpo slim kwenye fani,*
*no one can try me m*@#$k you better run.*


***Kiitikio x 2***
*Nani anafyum uswazi hakuna mipasho,*
*Hizi ni ngumu kwenye booth sokoni commercial,*
*Hizi ni bum kubam, bu bu kubam*
*kubum kubam, bubu kubam,*

***Ubeti 3***
*Leo Punchline zinabatizwa*



*kuwarudisha nyuma kwenye roots,*
*Niki pozi ni black (too black),*
*uswazi tunaishi kwa yeyo tuwe ma*
*lords kwenye banks,*
*it's like Bum kubam we call it bumbaks,*
*na hizo ndio ala ngumu,*
*tamu kama ngararum kwa wachaga*
*na push ndio warawararum,*
*kudumisha chama cha weusi kidumu,*
*tunatumia muda mrefu kubuni,*
*wanachukua kiulanii hawa baboon,*
*mangi si mangi duh,*
*wanasifiwa kwa swagga za kudu*
*duplicate, ingiza tape kwenye deck,*
*press record na dial code kwa lawyer to*
*communicate, yeah damn pilot,*
*twendeni kwenye market, I make*
*record for the record check crowd*
*reaction,*
*and this is A city monster*
*(Muungurumo wa samba)*

***Kiitikio***




## Na huu ugonjwa nao shida

Kuna mgonjwa mmoja alikwenda hospitali kupimwa, alipopimwa na dokta akagundulika anaumwa ugonjwa wa kiharusi mambo yakawa hivi:-

**DOKTA:** "Nimekupima nimekuta unaumwa Kiharusi"

**MGONJWA:** "Ni kweli dokta ndiyo mana nilikuwa nina hamu sana ya kutaka kuoa! Kumbe naumwa kiharusi"

Dokta alibaki anashangaa!



## Ulevi noma!

Mlevi kakutwa akikojoa eneo la shule, mwalimu akamuuliza hilo bango linasemaje? Mlevi akajibu: USIKOJOE HAPA. Mwalimu: kwa hiyo hapo unafanya nini?! Mlevi: kutoka moyoni nilijua hilo ni jina la hii shule.



## Huyu naye!

Jamaa aliamua kumtoa mkewe out..! kwaajili ya chakula cha usiku. kufika hotelini wakakaa mezani mhudumu akaja, kaka nikuhudumie nini? Tafadhali; niletee 'menu', Dada na wewe? Dada akajibu kwa pozi tena kwa kujishaua; "Na mimi niletee Menu ila usiweke chumvi nyingi"


## Pesa ndiyo kila kitu

Mume alimtumia ujumbe mke wake ikawa hivi;
Samahani mke wangu naomba unifulie nguo zangu zile nilivaa juzi na uzipige pasi.'
Muda ukapita mke hakujibu...mume akatuma sms nyingine: 'Pia nilisahau kukuambia kuwa hapa ofisini nimeongezewa mshahara mara tatu ya mwanzo na nimekununulia zawadi ya gari.'
Haikuchukua sekunde mke akajibu: 'Wow Unasema kweli mume wangu?
**Mume:** 'Nakutania tu, nilitaka kujua kama ile sms ya kwanza uliipata



# Umoja ni nguvu! Itumieni

Hali ya maisha imekuwa ngumu mpaka kesho haisomeki. Kila siku unahangaika huku na kule ilimradi upate chochote. Hakuna mwenye afadhali, kila mtu analalamika kuwa pesa imepotelea mbali, pesa imeota mbawa! Huyu hapa amejiajiri katika biashara lakini mambo bado, yule jembe naye karudi kuchakarika shambani lakini hana mtaji wa kueleweka, mwingine amekata tamaa hajui pa kuanzia. Kama umehangaika muda mrefu peke yako na huoni mabadiliko, kwa nini uendelee kuwa kivyakovyako? Kujitenga kwako kunakukosesha taarifa na fursa muhimu kwa kiasi kikubwa. Ndiyo! Kidole kimoja hakivunji chawa! Jiongeze!




## Je, wajua?

Kuna pesa ambazo zinatengwa kila mwaka katika kila wilaya kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujikwamua kimaisha. Na pesa hizi hutangazwa kwenye bajeti ya halmashauri kwa kupitia mabaraza yake. Kwenye haya mabaraza kuna madiwani ambao ni wawakilishi wa wananchi, na vijana wanaweza kuwatumia ili kupata taarifa za bajeti ya eneo wanaloishi.


## Jinsi ya kupata pesa hizi

- Andaa mchanganuo wa mradi
- Kikundi/ mtu kujaza fomu za kuombea pesa
- Vikao vya halmashauri vikae ili kupitisha mradi ulioainishwa katika mchanganuo wa kuombea pesa.
- Kuukagua mradi unaoombewa pesa
- Mwanasheria lazima aangalie mchakato mzima.
- Kisha pesa zinapitishwa kwenye akaunti ya benki



## Nani anastahili mkopo huu?

- Kijana yeyote wa Kitanzania mchapakazi/ anayejishughulisha
- Muaminifu na muadilifu
- Anayetambulika eneo la makazi yake
- Kijana aliye peke yake au kikundi cha vijana.




## Kwa nini muwe kwenye kikundi?

- Vikundi vinapewa kipaumbele katika kupata mikopo
- Ni rahisikumuwajibisha au kumkumbusha inapotokea mmoja wa wanakikundi kulegalega kulipa mkopo.



Afisa vijana wa Ilala, Emaculate Bachubire anafafanua, "Tunafuatilia mradi kila baada ya miezi miwili, na pia tunawapa kipindi cha makusanyo kuendana na aina ya mradi wanaoufanya" anaendelea kueleza kuwa riba ni 15% na masharti yake ni nafuu.

## Unapata mkopo;

Ndani ya miezi mitatu mkopo unaweza kupatikana, Japo wakati mwingine hutegemea na mapato ya Halmashauri husika.

## ☺ Kumbuka

*Kuwa na taarifa ni hatua ya kwanza ya mchakato. Mtembelee afisa vijana ili upate taarifaza mambo muhimu yanayohusu vijana.*

# Baba kijacho, linda chako!

"Yule si Mwajabu!? Kabeba mimba!!? Haya ni majanga! Binti kaumia halafu bado anajiongezea kidonda kingine? Daah! Kweli kuna watu hawajui kujihurumia" Maneno anasikia akiwaambia wenzake kuhusiana na hali ya Mwajabu. Maoni yake yanatokana na kufahamu kuwa Mwajabu ana maambukizi ya VVU. Kwa ufahamu wa Maneno, mwanamke mwenye VVU hastahili kubeba mimba kwani si salama kwa afya yake na mtoto.

Hiki ni kitendawili kikubwa katika jamii, hasa kwa wanaume ambao ufahamu wao juu ya masuala ya uzazi ni mdogo na hivyo kupelekea unyanyapaa kwa wajawazito wenye maambukizi ya VVU. Matokeo yake ni kupoteza watoto kwa sababu ya kukosa ufahamu sahihi.

### Inawezekana mtoto kuzaliwa salama?

Ndio, kama baba na mama watazingatia njia za kumlinda mtoto dhidi ya maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Kwa hiyo wake kwa waume jamii wanapaswa kuelimishwa kushirikiana kutumia huduma zaidi waweze kufahamu namna ya kutunza ujauzito na kumlinda mtoto.

Zipo njia ambazo wenzi wakizitumia kwa pamoja wanaweza kumkinga mtoto asipatwe na maambukizi ya VVU.




### Imani potofu

- Si sahihi kwamba ushiriki katika huduma za kuzuia maambukizi, kutamaanisha mmoja wenu ana VVU.

### Kwako Ba'kijacho!

Kuhusika katika uzazi salama ni muhimu sana, jamii inakuangalia kama kiongozi wa familia yako. Mwenza wako anataka kwenda Kliniki inabidi uhusike, mwenza wako anahitaji lishe bora, inabidi uhusike. Usione noma

Nenda na mwenza wako kliniki ili kupata ushauri nasaha juu ya kuishi na maambukizi ya VVU, lishe na namna ya kuzuia maambukizi mapya.

Pata Elimu ya namna ya kumkinga mtoto asipate maambukizi ya VVU. Elimu hii utaipata kutoka katika vituo vya afya. Pia mafunzo juu ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha.

### ☺ Kumbuka

*Mwanaume! Eeh! Afya ya mama na mtoto ni jukumu lako pia.*

# Kweli inawezekana!

Jerry na Maryam walijaaliwa kupata mtoto mmoja na walipotaka kumpata mwingine, walipima VVU wakakutwa wana maambukizi. Hawakutaka kuijulisha familia kwamba wanaishi na VVU. Kama ambavyo ni hiyari kwa mtu kupima, ni hiyari pia kwa mtu kuweka wazi majibu yake. Jerry na Maryam walifuata ushauri wa watalaam wa afya na mtoto alizaliwa bila maambukizi.

### Fahamu hili pia

Kwa kawaida, damu ya mama na mtoto akiwa tumboni havichanganyiki isipokuwa, maambukuzi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yanaweza kutokea kwenye hatua tatu:

- Wakati mtoto akiwa tumboni; endapo kondo la nyuma la mama limejeruhiwa, labda kutokana na kupigwa, kuanguka n.k, hivyo linaweza kupitisha maji maji yenye VVU kwenda kwa mtoto.
- Wakati wa kujifungua; kuingiwa na majimaji ya ukeni au majimaji mengine kutoka kwa mama sehemu zenye michubuko
- Wakati wa kunyonyesha, ambapo virusi vinaweza kuambukizwa kupitia maziwa anayonyonya




### Zingatia ushauri huu

- Zipo dawa zinazoweza kupunguza uwezekano wa mjamzito mwenye VVU kumwambukiza mtoto akiwa tumboni na wakati wa kujifungua. Nenda katika kituo cha afya kwa ushauri zaidi.
- Ni vyema kwa wenzi kupima VVU kabla ya mama kupata ujauzito.
- Ni vyema mjamzito mwenye VVU kuwa wazi kwa mshauri ili asaidiwe kujifungua salama
- Magonjwa ya ngono ni hatari kwa kila mtu lakini ni hatari zaidi kwa mjamzito mwenye VVU kwani yanaongeza uwezekano wa mtoto kuambukizwa.

### Kumbuka

*Maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yanaweza kuzuiwa endapo mama atawahi kliniki. Dawa za kuzuia maambukizi kwa mtoto hutolewa bure. Pia mjamzito mwenye VVU anatakiwa ajifungulie kwenye kituo cha afya na azingatie ushauri wa wataalam wakati wa kunyonyesha.*

# Wewe ndo bosi wa mwili wako

Leo yamemfika Nia. Hatimaye amempa kijana Kala kile anachotaka, bila kuwa na uhakika na anachokifanya kama ni sahihi au la. Nia na Kala, ni wapenzi kwa miezi kadhaa. Nia amekuwa akipokea pesa za matumizi madogo madogo kutoka kwa Kala. Jamaa amemnunulia hadi simu ya mkononi.

Lakini Nia hakuwa tayari kufanya ngono, alitaka wasubiri kidogo. Kala akamtisha kuwa kama hawatafanya ngono, atajua kuwa hampendi na atamuacha. Kwa shingo upande Nia akaona afanye anachotaka Kala ili asipoteze penzi na vizawadi toka kwa Kala.





## Hakuna cha bure

Kuna msemo unaosema 'hakuna cha bure'! Unaweza kudhani Nia analazimika kufanya ngono na Kala kwa sababu amekuwa akipokea zawadi na pesa zake lakini ukweli ni kuwa Nia ndiyo bosi wa mwilli wake, kwa hiyo hata akipewa zawadi, yeye mwenyewe ndiye anayetakiwa awe na maamuzi ya mwisho juu ya mwili wake.



## Kila mtu ana haki ya kusema hapana

- Watu wengi wanatumia fedha na zawadi kuwashawishi wenzao wakubali kufanya ngono. Kama hujaridhia sema HAPANA.
- Ni mwili wako na wewe ndiye mwenye uamuzi nao. Fanya maamuzi sahihi.
- Sema HAPANA ukimaanisha!

## Njia za kusema HAPANA kwenye ngono

- Unaposema HAPANA muangalie machoni huyo unayemwambia, kisha tumia sauti ya msisitizo kusema maneno hayo.
- Kama mpenzi wako atasema inaonekana humpendi kwa sababu hutaki kufanya naye ngono, mweleze ajue kwamba mapenzi ya kweli hayamaanishi kufanya ngono.
- Epuka vilevi kwani vinashusha uwezo wako wa kufanya maamuzi sahihi.
- Usifanye ngono kwa sababu tu mtu anataka mfanye. Hapana, wewe ndo mwenye maamuzi.
- Epuka sehemu za faragha ili kuepukana na vishawishi vitakavyokufanya uchukue uamuzi usio sahihi.

## Fahamu haya

- Mtu anayekulazimisha kufanya ngono wakati hukuridhia, anatenda kosa la jinai, hata kama alikuwa anakupa zawadi!
- Hata kama mtu amekuwa anakupa zawadi na kukufanyia vitu mbalimbali, haimaanishi ana haki ya kufanya ngono na wewe.

## ☺ Kumbuka

*Una haki ya kusema HAPANA! Hasa kwenye ngono. Ni mwili wako, utunze na usimruhusu mtu yeyote akufanyie maamuzi.*

# LAMBALAMBA

Sakata hili ni gumzo kila mahali na iliwakera kikundi cha vijana fulani katika Wilaya flani. Wamesema mengi lakini walibaki midomo wazi walipoachwa solemba bila malipo baada ya kufaya shughuli flani na taasisi husika. Fuatilia kisa hiki


*Michoro: babatau cartoons 2013*


















KUNA KAZI NYINGI ZA KUELIMISHA WATU HUKO VIJIJINI TUTA FANYA KWA PAMOJA NA KIKUNDI CHENU!
DAH! WASHKAJI MI HATA SIAMINI!
HILO ZALI MWANA... HAPO NDO MWAKE!
SHOSTI, SASA NI KAZI TU!
BAADA YA SIKU KADHAA
WAKUSANYE WASANII WENZAKO MJE HAPA OFISINI KWANGU LEO MSIKOSE!
ONESHO LITAFANYIKA KATIKA VIWANJA VYA MCHANGANI PALE KIJIJINI, NATUMAINI HAMTANIANGUSHA... HAYA NENDENI MKAJIANDAE KWANI KILA KITU KIMEKAMILIKA!
TUNASHUKURU KWA KUTUAMINI NA KUTUSAPOTI
KWELI
SIKU IKAWADIA, SAFARI YA KUELEKEA KIJIJINI IKAANZA
INABIDI TUKAMUE KICHIZI WASHKAJI NAFASI NDO HII!
NDO MAANA YAKE!
MWANANGU UMEIONA ILE SHOO IME BAMBA ILE KINOMA!
MCHIZI NIME HAMASIKA NAMI KUFANYA SANAA...
BAADA YA ONESHO...
KUHUSU PESA MTALIPWA TUKIRUDI WILAYANI... HAPA HAKUNA USALAMA!
MH! HATA KIANZIO! HAMNA


SIKU ZIKAPITA BILA KUPATA MALIPO YOYOTE...
TANGU TUMERUDI HUTU OFISA HAPOKEI SIMU, SASA MNAFIKIRI TUFANYEJE ILI KUPATA MALIPO YETU?
MI NAONA HILI CHANGA LA MACHO!
WAKAAMUA KUMFATA OFISINI KWAKE
SISI NI WASANII WA KIKUNDI CHA UBUNIFU TUNAFATILIA MALIPO YETU TUNAOMBA KUONANA NA AFISA WA VIJANA...
NANI ALIYEWA RUHUSU KUJA OFISINI MOJA KWA MOJA! MPIGIENI KWANZA SIMU YAKE!
TUMEPIGA SIMU YAKE MARA NYINGI HAPOKEI!
EBU ONDOKENI HAPA NI MAHALA PA KAZI MSILETE USUMBUFU! TUMEELEWANA?
WASHKAJI MI NAONA HAPA KAMA KUNA CHEZO LINA CHEZWA...
CHA MSINGI HAPA TUJIPANGE UPYA ILI TUIMARISHE KUNDI LETU LISIFE KAMA MENGINE
ANAYETAKA ABAKI ASIYE TAKA ASEPE!
TUJIAMINI TU JAMANI USANII NI KAZI KAMA ZINGINE...
MI NIMEFIKIRIA TUPANGE KWENDA KUMUONA BOSI WAO KWA VYOVYOTE, TUUNGANE TUSIKUBALI JASHO LETU LIPOTEE!
HIYO SAWA
POINTI
WAKAFANIKIWA KUMUONA AFISA WA NGAZI YA JUU
HILI SUALA NTALISHUHULIKIA MWENYEWE LAZIMA MPATE HAKI YENU, HII HAIKUBALIKI LAZIMA TUKEMEE VITENDO HIVI KWA NGUVU ZOTE!
VIJANA HATUTAKIWI KUKATA TAMAA...
LAZIMA TUUNGANE KUDAI HAKI YETU...
Vijana wengi hukata tamaa mapema kabla kupata mafanikio. Hawa wamedhulumiwa na kubaki wakilaumu kimya kimya. Chukua hatua hadi kieleweke!

# Mambo haya si mambo

Kila shughuli ina changamoto zake lakini nyingine ni za kujitafutia. Kwenye Mchezo huu wa katuni tunaona vijana ambao wanajishughulisha na uelimishaji kwa kutumia sanaa ya uigizaji. Wako tayari kujitolea kufanya shughuli za kijamii lakini pale inapotokea kuahidiwa malipo wanafurahi pia kwani shughuli yao hiyo ndiyo chanzo chao cha mapato. Tatizo linakuja pale mtu anapowaahidi kuwalipa lakini hawalipi.




**Kuna mitazamo tofauti kuhusu sababu...**

Fikiria umeahidiwa malipo endapo tu utafanikisha kazi fulani halafu mwisho wake unazungushwa hadi unakata tamaa. Tumezungumza na baadhi ya vijana wa huko Arusha juu ya suala hili na haya ni machache waliyoyaeleza

- Inawakatisha tamaa vijana kujiunga na sanaa ya kuigiza au kuanzisha vikundi vya sanaa.
- Kutokuwa na imani na taasisi, mtu binafsi n.k kwa shughuli nyingine zijazo.
- Kusambaratisha vikundi vichanga katika fani husika
- Kujenga chuki baina ya viongozi wa kikundi na wanachama
- Kujenga chuki baina ya vikundi vya vijana na viongozi wa taasisi husika ya aliyeahidi malipo.

**☺ Kumbuka**

Vijana wanahitaji mwongozo bora wa heshima na uaminifu katika maisha ili kutimiza malengo wanayojiwekea kila siku.

# Fungu hili limekaaje?

Kwenye Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo, kuna fungu linalotolewa kila mwaka wa fedha, lenye lengo la kuendeleza vijana chini ya "mfuko wa maendeleo ya vijana. "Pesa hizi hupelekwa wilayani kama ruzuku kutoka serikalini kupitia kitengo cha maendeleo ya vijana. Hutolewa kwa vijana kwa njia ya mkopo, wenye masharti nafuu. Pesa hizi japo ni kidogo, lakini ni muhimu ukaziulizia na kupeleka maombi kwenye kitengo husika.




### Fungu lina shilingi ngapi?

- Kila mkoa unatakiwa kukusanya mapato kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za mkoa.
- Mapato haya hutokana na vyanzo vya ndani ya mkoa
- Ni jukumu la kila mkoa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwenye mfuko wa maendeleo ya vijana.
- Pia kuna fungu (ruzuku) ambayo hutoka serikali kuu kwenye Wizara ya Vijana, ambalo hutangazwa kila mwaka wa fedha. Fungu hili huwasilishwa kwenye mkoa husika kisha kupelekwa katika kila wilaya, kitengo cha maendeleo ya vijana.




### Masharti ya fungu hili

- Spesho kwa ajili ya wanawake na vijana.
- Hutolewa kwa vijana kwenye vikundi lakini hata kijana mmoja mmoja anaweza kupewa ilimradi itimize masharti.




## Ushauri

- Usikate tamaa, tembelea ofisi ya maendeleo ya vijana, zipo kwenye kila wilaya/mkoa na tafuta taarifa sahihi kuhusu mfuko huu.
- Tuwe waaminifu hasa katika kutumia pesa hizi kwenye kujikwamua na ugumu wa maisha
- Nidhamu na uadilifu katika kutumia mikopo hiyo likiwemo suala la vijana kurejesha kwa wakati mikopo ni suala muhimu na la kuzingatia

## Kazi ya fungu hili ni lipi?

- Kusaidia vijana au vikundi vya vijana ili waweze kujiajiri kupitia shughuli za uzalishaji mali na miradi ya kiuchumi.
- Kupunguza ukali wa maisha kwa vijana ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

## Swali

**Je, unadhani pesa inayotolewa inakidhi mahitaji ya vijana kwenye wilaya nzima?**
**Kujibu kwa SMS; Andika SM acha nafasi andika 66 acha nafasi kisha andika jibu lako tuma kwenda 15665**




# Shindano la Ruka Juu! na Fema TV Show linaendelea kwa kishindo. Mpe shavu mshiriki umpendaye kwa kumpigia kura!

Dirisha la kupiga kura linafunguliwa Jumamosi saa 1 jioni na kufungwa Jumanne saa 5 na dakika 59 usiku...ZINGATIA HILO!

Kumpigia TATU kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 4
tuma kwenda
**15665**





Kumpigia MUSTAPHA kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 1
tuma kwenda
**15665**

Kumpigia YUSTA kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 5
tuma kwenda
**15665**





Kumpigia LAWRIANI kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 2
tuma kwenda
**15665**

Kumpigia JOSEPH kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 6
tuma kwenda
**15665**





Kumpigia AZIZA kura,
andika **RUKA** acha nafasi
andika 3
tuma kwenda
**15665**

Usikose kuangalia luninga yako

ITV kila J'mosi saa 1 jioni
(Marudio J'nne saa 7 mchana)

TBC1 kila J'pili saa 4 usiku
(Marudio J'mosi saa 6 mchana)

Funguka shambani peta maishani na Fema Radio

RFA kila J'tatu saa 2:45 usiku

TBC FM kila J'nne saa 3 usiku

# USHAURI

## Swali

Nimekaa saluni, mume wangu anajadiliwa na wasichana waliopo hapo saluni. Hawajui kama mimi ndiye mkewe. Msichana anayetembea naye anaongea na mume wangu kwenye simu. Namsikia mume wangu anajiachia tu. Hajui kama kawekwa 'loud speaker'. Wanakata simu wanacheka sana! Mbaya zaidi, wanasema jamaa ananiponda ile mbaya, wanataja na mapungufu yangu ambayo kwa asilimia kubwa ni ya kweli. Je, nifanyeje?

*Msomaji Geita*

Nashukuru kwa swali pia kwa uvumilivu. Kama unampenda mumeo kaa naye kwa ustaarabu mweleze kisa kilicho kutokea saluni halafu uone anasema nini. Jibu atakalo kupa litafakari kabla hujajibu kama ukiona unaogopa kumuuliza ni vyema uwaeleze wazee wenye busara au mshenga wako ili waweze kukusaidia.

Ukinyamaza kimya haitakusaidia Waswahili husema; "dawa ya jipu nikulipasua". Kuwa muwazi ili kujenga mahusiano ya nyumba yenu.




Napenda kukuambia kwamba usipende kusikiliza maneno yanayosemwa na watu, ila kaa chini uchunguze kwa makini. Je ni kweli aliyekuwa anazungumza kwenye simu ni mume wako au ni mtu mwingine, si unajua duniani watu hutokea kufanana.

*Naimi Obedi*

*Arusha – Mianzini*


Mwanamume kutaja mapungufu yako sio kwamba hakupendi, ni njia mojawapo ya kumpata huyo msichana anayeongea naye. Cha muhimu hapo ni kumrudisha kwenye himaya yako ili asitangetange, pia acha kuwa na hisia za kujidharau ili jamaa aweze kutulia.



*Frank Kimaro*

*Arusha*

Dada yangu nakushauri uvute subira na kama ikibidi ungetumia nafasi hiyo kuchunguza mengine pia kupitia hao wadada wa saluni. Pia ni muhimu ukaenda kupima ili kujua afya yako na ikibidi uambatane na mumeo bila kumwambia hiyo sababu. Unaweza tumia sababu nyingine kwani baada ya kupima afya yako utaweza kujilinda zaidi. Pia ni muhimu kuwaona viongozi wa dini ili waweze kusikiliza hilo shauri.



*Roy Reuben*

*Arusha*

### SWALI LA TOLEO LIJALO

Mimi nina shida, naomba ushauri kwa wenzangu. Mimi ni msichana wa miaka 30, nimeolewa. Nampenda na namheshimu mume wangu. Tatizo ni kaka yake. Amekuja mjini mwaka mmoja uliopita kutafuta kazi na hadi leo anasema hajapata. Tunaishi kwenye chumba kimoja na sebule na tunaishi naye kwa mwaka mzima sasa. Kusema kweli nimechoka. Nahitaji kufurahia ndoa yangu. Anatubana na nakosa uhuru na faragha. Mume wangu naona anashindwa kumwambia kaka yake aondoke japo anajua sifurahii tena uwepo wake. Nimeamua nifungashe vilivyo vyangu niondoke au yeye aondoke. Tafadhali naomba ushauri.

*Msomaji wa Si Mchezo!*



**Betty Liduke ni rafiki mkubwa wa vijana, hata wewe unaweza kulonga naye. Ni msambazaji mkubwa wa Jarida la Si Mchezo! Mkoani Njombe. Ni mshauri nasaha na ni Mratibu wa Kitengo cha Udhibiti Ukimwi katika Kampuni ya TANWAT, Njombe.**

**Mwandikie kupitia Jarida la Si Mchezo!**
**Si Mchezo!**
**S. L. P. 2065**
**Dar es Salaam**

SMs; Andika **SM** acha nafasi, andika maoni yako kisha tuma kwenda namba **15665** **na utuambie kama ungependa uchapishwe.**

# Wazazi nipendeni




***Tuma SMS neno "mtoto" BURE kwenda 15001 kwa taarifa zaidi***

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii